TANGAZO LA SERIKALI NA. 224 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA AFYA, USAFI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 297 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ya Mwaka 2024 ambazo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa-

(a) kufuta tafsiri ya neno "taka ngumu" na kuiandika upya kama ifuatavyo:

Sura ya 191

""taka ngumu" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;"; na

(b) kuongeza kulingana na mpangilio wa kialphabeti tafsiri ya msamiati mpya kama ifuatavyo:

""viwanda" maana yake ni-

(i) kwa kiwanda kidogo,

kiwanda chenye mtaji wa zaidi ya milioni tano hadi milioni mia mbili na waajiriwa kuanzia watano hadi arobaini na tisa;

(ii) kwa kiwanda cha kati, kiwanda chenye mtaji wa zaidi ya milioni mia mbili hadi milioni mia nane na waajiriwa kuanzia hamsini hadi tisini na tisa; na

(iii) kwa kiwanda kikubwa, kiwanda chenye mtaji wa zaidi ya milioni mia tano na waajiriwa kuanzia mia moja na kuendelea;".

Marekebisho ya kanuni ya 6

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6(2), kwa kupangilia upya aya ya (j) kuwa maneno ya kufungia.

Marekebisho ya kanuni ya 7

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 7-

(a) katika kanuni ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "tarehe 30 ya kila mwezi" na badala yake kuweka maneno "tarehe ya mwisho wa mwezi"; na

(b) katika kanuni ndogo ya (3), kwa kuingiza maneno "bila kuwa na sababu ya msingi" katikati ya maneno "mfululizo" na "Halmashauri".

Marekebisho ya kanuni ya

5. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 19 kwa-

19

(a) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(b) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (1) kuwa kanuni ya 19.

Marekebisho ya kanuni ya 27

6. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 27 kwa-

(a) kufuta aya (i); na

(b) kubadili mpangilio wa aya (j) hadi (n) kuwa aya ya (i) hadi (m) mtawalia.

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*